

# Mfumo utoaji vibali kielektroniki wazinduliwa

Na Grace Mwakalinga,  
MBEYA

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imezindua mfumo mpya wa utoaji vibali kielektroniki kusafirisha mifugo na bidhaa zote zitokanazo na ngozi ili kuondoa urasimu, rushwa na uzembe uliokuwa unafanywa na baadhi ya wataalamu wanaoshughulikia upatikanaji wa vibali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Tixon Nzunda, alisema jana kuwa mfumo huo itaanza kutumika rasmi Julai

mosi, mwaka huu.

Alisema mfumo huo utarahisisha shughuli za utoaji vibaji kwa njia ya mtandao na wafanyabiashara hawatapanga foleni kwa wataalamu wakiwamo maofisa ugani kushughulikia vibali vya kusafirisha mifugo na mazao yatokeanayo na mifugo badala yake watatumia teknolojia za simu na kompyuta kuvipata.

Alisema serikali ilianzisha mfumo huo kuokoa na kukusanya mapato yatokanayo na ukataji wa vibali na kuwabana watumishi waliokuwa wakiendekeza rushwa na urasimu kuwahu-

dumia wananchi.

"Tunajivunia kuona sasa tume-fanikiwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki ambao utatumika kutoa vibali vya usafirishaji wa mifugo na bidhaa zake, kama vile ngozi, mayai na nyama kutoka kila pembe ya nchi huko aliko atapata kibali chake kupitia simu yake ya mkononi na kuen-delea na shughuli zake," alisema Nzunda.

Alisema wameamua kutambulisha mfumo huo kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hususani mkoani Mbeya kwa kuwa ni eneo ambalo linawafugaji wengi am-

baio wanafuga kisasa na kuzalisha maziwa yenye ubora unaokubalika kimataifa.

Kwa upande wake, Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Daniel Mushi, alisema mfumo huo utarahisishia wafanyabiashara wa nyama nchini kupata vibali kwa wakati na kufanya shughuli zao kwa uhuru. Alisema mfumo huo utapunguza mlolongo mrefu wa kufuatilika vibali katika ofisi za serikali na badala yake vitakatwa kielektroniki.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Trade Mark East Afrik, Lilian Masalu, alisema

walishawishika kuisaidia serikali kuanzisha mfumo huo baada ya kuona ucheleweshwaji wa vibali vya kusafirisha mifugo hali iliyokuwa inasababisha bidhaa zitokanazo na mifugo kuharibika na wafanyabiashara kuingia hasara.

Alisema mfumo huo utakuwa na tija kwa mfugaji na mifanyabiashara ambao kwa pamoja watazuza kwa wakati na kujing'zia kipato.

Baadhi ya wafanyabiashara wanaojishughulisha na uuzaji wa ngozi walisema mfumo huo utasaidia kuwa na bei ya pamoja nchini kuliko ilivyo sasa.

mikopo ya pikipiki na bajaji  
kwa lengo la kuwawezesha..